

## **A Wito wa kichungaji wa Paulo. Wagalatia 4:12.**

### ❖ **“Ndugu zangu, Nawasihi”**

- Kwanza Paulo anatoa wito kwa fahamu za Wagalatia, kisha anatoa ombi, wito kwa mioyo yao..
- Walikuwa watoto wake wa kiroho, lakini kazi yake ikanonekana kutokuwa na matunda kwa sababu ya mienendo yao. Ilibidi “awaonee utungu tena” ili waunganike na Kristo (Wagalatia 4:19).
- Walikuwa wameingilia ukuaji wao, hivyo iliwapasa kubadilishwa kabisa . Ilibidi Kristo “aumbike” ndani yao tena

### ❖ **“Iweni kama mimi”**

- Kipindi hiki anaenda zaidi ya kuiga tu. Kama wito wake kwa Agripa (Matendo 26:28-29), Paulo hakuwaomba Wagalatia kufanya kama yeye, bali kuwa kama yeye.

### ❖ Aliwataka wapate uzoefu wa maisha ya Kikristo aliyokuwa anaishi, furaha ile ile kwa wokovu, ushirika uleule katika Kristo...

### ❖ **“maana mimi ni kama ninyi”**

- Paulo alikuwa na kipawa cha utambuzi wa muktadha. . Alitumia njia tofauti kutegemea aina ya watu aliotaka kufikia.

**B** Alizungumza na wanafalsafa kwa hekima (Matendo 17:16-34). Aliwashawishi Wayahudi kwa tamaduni zao (Tazama Waebrania). Alizungumzia kuhusu msalaba wa Kristo kwa Wakorintho wasio na maadili (1 Wakorintho 2:2). Alikuwa Myahudi ila akawa Mmataifa ili kuwafikia Wagalatia.

## **C Kukumbuka Mianza. Wagalatians 4:13-15.**

- ❖ Paulo alipumzika Galatia kwa sababu ya ugonjwa wa jicho. Akatumia fursa hiyo kushuhudia imani yake mbele ya Wakorintho, waliompenda sana kiasi kwamba wangelitoa macho yao na kumpa kama wangeluweza (Wagalatia 4:15).Mwisho wa barua yake, Paulo anawaambia kwamba bado alikuwa na shida na macho yake (Wagalatia 6:11).

**D** Paulo anaelekeza katika hisia za furaha walizosikia Wagalatia walipojua kweli za Injili. Je hisia hizo zilikuwa zimetoweka?

## **E Kuusema ukweli. Wagalatians 4:16-20.**

- ❖ Paulo aliamua kuwakabili Wagalatia na mwenendo wao, hata kama hilo lingeharibu uhusiano wao.
- ❖ Azma yake ilikuwa safi. Aliwapenda sana kiasi cha kutotaka hata mmoja wa wana na binti zake katika Imani kupotea.
- ❖ Mtazamo wake ulipingana na ule wa waalimu waongo waliojaribu kupata upendeleo wa Wagalatia kwa sababu za ubinafsi (Wagalatia 4:17).